**WIZARA YA ELIMU**

**JIMBO LA KUSINI**

**WILAYA YA MUHANGA**

**MTIHANI WA MUHULA WA PILI WA WILAYA YA MUHANGA**

**MKONDO WA LUGHA, MCHEPUO WA LFK, KIDATO CHA TANO**

**TAREHE 25/3/2026 ALAMA: ……………../ 100**

**MAELEKEZO:**

**Jibu maswali yote,**

**Mwandiko wako usomeke vizuri**

**Usisahau kuandika vizuri nambari ya kila swali.**

## Tamaa mbele mauti nyuma

Siku hiyo, sote tulikuwa nyumbani. Jua liliaga miti na nuru ya mchana ikafifia. Anga ikavaa joho jeusi tititi kama kizimwili. Giza totoro likazagaa na kushamiri kote. Usiku ukashika hatamu na kutamalaki. Mimi na umbu zangu tulijipweteka pwete makochini. Baadhi yao walisikika wakitia chumvi porojo zangu kuhusu nia ya kakangu ya kujipatia jiko huku mama na mnuna wangu wakituandalia chakula. Muda mrefu haukupita kabla ya meza kujaa mapochopocho kochokocho na harufu nzuri kusikika kote sebuleni. Mara mchuano kati ya magego na mlo ukaanza. Mara kunyofoa minofu nyofu nyofu, mara kutafuna chapati sikwambii kugwengwenya mifupa!

Punde si punde, mambo yakatokea v uu. Kama ajali, tuligutushwa na kishindo kikuu kilichotisha kama Izraili. Sote tulituama na kuachama, tukabaki tumemaka. Nilinyanyuka na kusimama dede huku nikitetemeka tetete kama kifaranga aliyenyeshewa na mvua ya gharika katika msimu wa kipupwe. Nao wasiwasi wa mwasi ukanivaa kama libasi lakini nilipiga moyo konde. Kwa wayowayo na jakamoyo nilikwenda nyatunyatu na kutupa jicho. Kwetu na mahali penyewe palikuwa pua na mdomo. Viwiliwili vya watu wengi wenye kurunzi vilionekana vikikimbia mkikimkiki kuelekea barabarani.

Kumbe ni kweli, mbiu ya mgambo ikilia kuna jambo! Mara maneno tepetepe na mipayuko kama ya wehu ikatamalaki na kuhinikiza hewani. “Leta mitungi! Ondoka nichote! Hiki ni chanzo cha amani na

maendeleo ya kijiji chetu! Umaskini kwaheri! Ondoa ushamba, bwege wewe! Kila mtu anataka kuchota mafuta, usilete ubaradhuli!" Ndizo sauti zilizowakosesha watu usingizi.

Fumbo hufumbiwa mjinga mwerevu akatambua! Papo hapo, niling'amua kuwa vya bwerere vilikuwa vimepatikana. Nilighairi kubaki nyuma kama koti la mzee na kuamua kuwa wa mbele kama mfuko wa shati. Nani asiyejua kuwa aliye kando haangukiwi na mti? Nilinyakua mtungi na kufululiza kenyekenye hadi palipokuwa na umati wa watu. Nilipofika, watu walikuwa wakiangukiana. Wengine walifokeana ungedhani walikuwa na kamusi ya matusi vinywani. Wengi wao walikula mwande! Wengine walifanya kazi chapuchapu. Nami nilifanya kulihali lakini nikagonga mwamba.

Tukiwa katika pilikapilika za kuyateka mafuta ya bwerere, jamaa fulani njorinjori, mrefu kama mlingoti na mweusi tititi kama lami aliwasha sigara. Kwa kweli, lila na fila havitangamani! Kabla hajapuliza fundo la kwanza, mlipuko wa ajabu ulisikika. Lo! Lahaula! Moto mkubwa ulizuka zu kama mizuka na kuzidi kuenea! Kukurukakara za kujinusuru zilianza. Ikawa ni pata shika, nguo kuchanika na miguu niponye. Watu waligongana dafrau na kuangushana kama magari barasteni.

Kila mmoja alijaribu kuisalimisha aushi yake. Moto nao uliendelea kuwaka na kuchoma bila huruma. Maskini wanyonge waliteketea teketeke kiasi cha kutoweza kutambulika. Watu takriban hamsini walikata kamba na wengine kugeuzwa vilema. Niliponea katika tundu la sindano!

Kuona hivyo, niliikumbuka kauli ya wahenga kuwa "tamaa mbele, mauti nyuma". Maneno tamaa, pupa na papara niliyazika katika kaburi la sahau maadamu yanaweza kuwa chanzo cha balaa. Tangu siku hiyo, maisha yangu yalichukua mwelekeo mpya.

SEHEMU YA I: UFAHAMU NA MSAMIATI. ALAMA 25

Chagua jibu sahihi

1. Tukio kuu lililotokea katika hadithi ni gani? Alama 2
   **A)** Harusi ya kijiji
   **B) Mchuano wa kupata mafuta ya bwerere**
   **C)** Sherehe ya chakula
   **D)** Shughuli za kilimo
2. Methali gani ilitumiwa kuelezea hatari ya tamaa? Alama 2
   **A)** "Ndege aamkaye asubuhi hula wadudu watamu"

**B) “Tamaa mbele, mauti nyuma”**

**C)** “Haraka haraka haina baraka”

**D)** “Maneno mengi hayavunji mfupa”

3. Watu walijaribu kuokoa maisha yao kwa kufanya nini? Alama 2

   **A)** Kukimbia na kuogelea

   **B) Kukimbia na kuepuka moto**

   **C)** Kuimba na kuomba msamaha

   **D)** Kuchota maji kutoka mto

4. Moto ulizuka kutokana na nini? Alama 2

   **A)** Sherehe ya chakula

   **B) Ajali wakati wa mchuano wa kuchota mafuta**

   **C)** Mazingira ya mvua

   **D)** Mwanga wa jua

5. Ni nini kilichotokea kwa watu wengi baada ya moto kuwaka? Alama 2

   **A)** Waliokolewa wote

   **B) Wengi walikufa na wengine kuumia vibaya**

   **C)** Waliendelea kazi kama kawaida

   **D)** Walikimbia msituni

6. Mwandishi alipata mshtuko gani baada ya tukio la moto? Alama 2

   **A)** Alicheka na furahi

   **B) Alijifunza thamani ya methali za wahenga**

   **C)** Alipenda moto zaidi

   **D)** Hakujali kabisa

7. Methali “Tamaa mbele, mauti nyuma” ina maana gani? Alama 2

   **A)** Kuishi kwa furaha kila wakati

   **B)** Kupenda mali zaidi ya maisha yako

   **C) Kutaka kupata mali kwa kila hali hata kwa madhara**

   **D)** Kuogopa mauti na kutotaka kufa

8. Watu walijitahidije kushindana kuchota mafuta ya bwerere? Alama 2

   **A)** Kwa amani na utulivu

   **B) Kwa mchuano na mivutano mikali**

**C)** Kwa usaidizi wa mzee mmoja

**D)** Kwa kuomba baraka

9. Bainisha mafunzo mawili kutoka kifungu hiki cha habari. Alama 2

- ✓ Kufahamu kwamba ni lazima kutofanya jambo kwa tamaa kwani unaweza kukutana na madhara makubwa.
- ✓ Kujitahidi kufanya bila kutumaini kwamba utapata vya bure.

N.B: hapa kwenye swali hili, utasahihisha kulingana na maoni yaliyotolewa na mwanafunzi.

10. Memo '**Mbiu ya mgambo ikilia kuna jambo**' humaanisha: Alama 2

A. Tamaa ya kupita kiasi huleta hatari au maafa.

B. **Uvumi hauna kosa, kuna ukweli ndani yake**

C. Aliye na akili huelewa maana ya mafumbo

D. Hakuna jibu sahihi.

11. Chagua neno sahihi kutoka kisandukuni na kujaza nafasi wazi. Alama 5

| lila na fila, nyatunyatu, mauti, giza totoro, bwerere |
|---|

a) Wakati umeme ulikatika ghafla, nyumba nzima ikafunikwa na **giza totoro**

b) Yule mgonjwa alikuwa katika hali mbaya sana kiasi kwamba madaktari waliogopa kuwa **mauti** ingemfika muda wowote.

c) Watoto walitembea **nyatunyatu** wakijaribu kutokuamsha mbwa aliyekuwa analinda mlango.

d) Alienda sokoni na kupata matunda **bwerere** baada ya mfanyabiashara kufanya promosheni.

e) Mawazo ya ndugu hao yalikuwa **lila na fila**; hawakukubaliana kabisa kuhusu uamuzi wa familia.

SEHEMU YA II: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA. ALAMA 30

12. Kinyume cha neno "kubwa" ni ......... alama 1

a) Chache b) embamba c) nene **d) dogo**

13. Wengi walikufa. Neno "wengi" ni: alama 1

a) Kihisishi b) Kielezi c) Kivumishi **d) kiwakilishi**

14. Chagua jibu sahihi. Alama 2

a) Ikiwa leo ni Ijuma. Jana ilikuwa............. (Jumapili, **Alhamisi**, Jumosi).

b) Ikiwa kesho ni Alhamisi, leo ni ............. (Jumamosi, Jumanne, **Jumatano).**

15. Andika wingi au umoja wa maneno haya. Alama 2

a) Kioo kipya. **Vioo vipya.**

b) Matunda mabivu **Tunda bivu.**

16. Andika hali kanushi au yakinishi ya tungo zifuatazo. Alama 2

a) Mwalimu hufundisha wanafunzi. **Mwalimu hafundishi wanafunzi.**

b) Usiende nyumbani. **Nenda nyumbani.**

17. Sahihisha sentensi hizi. Alama 2

a) Kalamu haandiki vizuri. **Kalama haiandiki vizuri.**

b) Tungelijifunza kwa bidii, tungeshinda mitihani. **Tungelijifunza kwa bidi, tungelishinda mitihani.**

18. Tunga sentensi ukitumia neno "–zuri" kama: Alama 2

a) Kiwakilishi **Mzuri anapendwa.**

b) Kivumishi **Mtoto mzuri anapendwa.**

19. Tumia kivumishi kilichoko kwenye mabano kukamilisha sentensi. Alama 2

a) Mwimbaji anaimba **vibaya** (-baya).

b) Juma ana mapapai **mengi** (-ingi).

20. Kamilisha sentensi hizi. Alama 2

a) Ungeniambia, **ningefahamu kwamba ni hatari ya maisha yangu.**

b) Mitihani isingelikuwa rahisi, **wanafunzi wangelishinda vizuri.**

21. Andika usemi wa taarifa wa sentensi hii. alama 2

- 'Mtafanya jaribio kesho', mwalimu aliwaambia wanafunzi.

**Mwalimu aliwaambia wanafunzi kwamba wangefanya jaribio siku ambayo ingefuata.**

22. Jaza na: -ingine. Alama 2

a) Nahodha **mwingine** hajui Kifaransa.

b) Maua **mengine** yamekauka.

23. Jaza pengo na -enye. Alama 2

a) Mipera **yenye** majani mengi ni ile ile.

b) Papai **lenye** mapapai matamu ni la bibi.

24. Jaza pengo. Alama 2

Kwa mfano: Mume ni kwa mke na mvulana ni kwa msichana.

a) Mfalme ni kwa **malkia** na **dada** ni kwa kaka.

b) Nyanya ni kwa **babu** na shangazi ni kwa **mjomba.**

25. Ondoa amba- katika sentensi hizi bila kubadili maana. Alama 2

a) Wanafunzi ambao wanasoma kwa bidii. **Wanafunzi wanaosoma kwa bidi.**

b) Kitabu ambacho kiliibwa na watoto. **Kitabu kilichoibwa na watoto.**

26. Ainisha sentensi zifuatazo. Alama 2.

a) Viongozi wote ulimwenguni ni watumwa ni watumwa wa raia. **Sentensi sahili.**

b) Dada anasafisha nyumba na anasikiliza matangazo. **Sentensi ambatano.**

27. Dhihirisha kiima na kiarifu katika tungo zifuatazo. Alama 2

a) Mtoto mwenye tabia nzuri hupendwa.

**Mtoto mwenye tabia nzuri ni** kiima **ingawa** hupendwa ni **kiarifu.**

b) Sisi tulipikwa chakula na mtu mwenye ujuzi kabisa.

**Sisi: kiiima lakini** tulipikiwa chakula na mtu mwenye ujuzi kabisa ni **kiarifu.**

SEHEMU YA III: FASIHI (ALAMA 30)

28. Sema ndiyo au hapana. Alama 5.

a. Ili kazi ya fasihi iingizwe katika fasihi ya Kiswahili ni lazima izungumzie utamaduni wa Waswahili na itungwe katika Kiswahili. **Ndiyo.**

b. Kazi za sanaa za fasihi ya Kinyarwanda au ya Kirundi au ya Kiingereza zikiandikwa kwa Kiswahili zinaweza kuitwa kazi za fasihi kwa Kiswahili. **Ndiyo.**

c. Ili fasihi simulizi ya Kiswahili iendelee kuwepo, ni lazima lugha ya Kiswahili isitumiwe kwa ufasaha ili kupambana na lugha za kikoloni. **Hapana.**

d. Wanafasihi husema kuwa "nahau" ni semi amabazo hudai kitenzi maalumu ndani yake ili ziwe na maana ilhali "misemo" ni semi ambazo hazidai vitenzi ili ziwe na maana. **Hapana.**

e. Mimi na ndugu yangu tulinunua fahali mmoja kutoka sokoni. Baada ya mwaka mmoja alijifungua ndama wawili. Je, kila mtu alipata wangapi? Huu ni mfano wa kitendawili. **Hapana.**

29. Fasihi hulinganishwa na kioo cha jamii. Eleza kauli hiyo ukitoa mifano anuai.

**Kama tunavyojua fasihi ni sana imulikayo hisia, mawazo na malengo ya jamii kwa kutumia lugha. Ilhali jamii ni kundi la watu waishio katika sehemu moja, wazungumziwayo lugha moja pamoja na utamaduni mmoja. Tukumbuke kwamba kioo ni kifaa cha kujiangalilia sura yako. Ni kwa hivyo ni kioo cha jamii kwani ndiyo inarithisha na kudumisha mila na desturi za wanajamii fulani.**

30. Unganisha nahau zifutazo na maana zake. Alama 5

| Nahau | Maana | Majibu |
|---|---|---|
| a) Kugomba mwamba | i. Kuwa makini; tahadari. | ⟹ a) **iii.** |
| b) Kukata Kamba | ii. Wazi kabisa | ⟹ b) **v** |
| c) Dhahiri shahiri | iii. Kutofanikiwa | ⟹ c) **ii** |
| d) Cheza na moto | iv. Fanya jambo la hatari. | ⟹ d) **iv** |
| e) Fungua macho | v. Kufariki | ⟹ e) **i** |

31. "Kumwaga unga" humaanisha nini? Alama 2

a) **Kufukuzwa kazi au nafasi**

b) Kula vibaya

c) Kutema chakula

d) Kupika kwa hasira

32. "Kumezea mate" inahusiana na nini? Alama 2

a) Kula chakula kingi

b) Kucheua baada ya kula

c) **Kutamani kitu au mtu**

d) Kuumwa na meno

33. Chagua neno sahihi kutoka mabanoni na kuzaja nafasi wazi. Alama 4

a) Aisifuye ......., imemnyeshea. (jua, mawingu,**mvua**)

b) ........ hufuata upepo. (miti, **bendera**, maua)

c) Usitukane ......... na uzazi ungalipo. (**wakunga**, wazazi, walimu)

d) Mwezi na mtembezi, ......... na mwizi. (**giza**, kisu, bunduki).

34. Methali: "Tembo hashindwi na mkonga wake" ina maana gani? Alama 2

a) Tembo hawezi kutembea bila mkonga

b) **Mtu hawezi kushindwa na jambo linalomhusu mwenyewe**

c) Tembo hutumia mkonga kula tu

d) Mkonga ni silaha ya tembo

35. Methali: "Teke la kuku halimwumizi mwanawe" ina maana gani? Alama 2

a) Kuku hawana hasira

b) **Mzazi hampigi mtoto kwa madhara**

c) Kuku humpa mtoto chakula

d) Mtoto halali jiko.

36. Methali: "Usitukane wakunga na uzazi ungalipo" inafundisha nini? Alama 2

a) Wakunga ni muhimu kwa jamii

b) Usikose shukrani baada ya msaada

c) **Usimdharau mtu ambaye bado unaweza kumhitaji**

d) Uzazi ni wa akina mama tu

37. “Mtu mwenye kasi hupoteza kila kitu kwa kutotulia.” haya yanalingana na methali: Alama 1

    a) Chelewachelewa utamkuta mtoto si wako.

    b) Akili ni mali.

    c) Bandu bandu humaliza gogo.

    d) **Mtaka yote kwa pupa hukosa yote.**

SEHEMU YA IV: UTUNGAJI. ALAMA 15

38. Chagua mada moja kati ya hizi mbili na kuizungumzia katika sentensi kati ya 25-30 - Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.

    - Madhara ya kuharibu mazingira
    - Jinsi ya kuhimiza usafi shuleni

SEHEMU YA UTUNGAJI

Hapa kwenye sehemu hii unapofanya masahihisho ya swali hili, chunguzeni haya yafuatayo:

- ✓ **Chunguza ikiwa ametumia muundo wa insha yaani mwanzo, kiini na mwisho. Alama 3**
- ✓ **Hoja zake zinazoeleweka. Alama 9**
- ✓ **Kichwa. Alama 1**
- ✓ **Matumizi ya sarufi yaani usanifiashaji wa lugha. Alama 2**

**BARIKIWENI NYOYE!!!!!! NAWATAKIA PASAKA NJEMA!!!!**

**MTAKA CHA UVUNGUNI SHARTI AINAME!!!**